# MUHTASARI WA UCHAMBUZI BAJETI YA WIZARA YA KILIMO

**2025-2026.**




WIZARA YA KILIMO

MINISTRY OF AGRICULTURE

# MUHTASARI WA UCHAMBUZI BAJETI YA WIZARA YA KILIMO

2025-2026.

## MAFANIKIO YA BBT KUZALISHA AJIRA MILIONI 1.08 UZALISHAJI WA AJIRA MILIONI 1.08 SEKTA YA KILIMO

"hadi kufikia mwezi April 2025, katika eneo la ajira zilizotokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo, Wizara imezalisha ajira za kudumu na za muda mfupi Milioni 1.08 kupitia programu na miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo ikiwemo miradi ya uzalishaji na utafiti; ujenzi, ukarabati na usanifu wa miradi ya umwagiliaji, programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora na Vyama vya Ushirika" Mhe. Hussein Mohammed Bashe, (Mb), Waziri wa Kilimo, Hotuba ya Bajeti 2025/2026.

### KUONGEZA AJIRA ZENYE STAHA NA USHIRIKI WA VIJANA NA WANAWAKE KWENYE KILIMO

Wizara katika kuhakikisha upatikanaji wa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tommorrow – BBT) inayotekelezwa kupitia miradi ifuatayo:-

1. **Mashamba Makubwa ya Pamoja (Block Farms) Shamba la Chinangali ekari 1,772**
    - Jumla ya vijana na wanawake 261 wamekabidhiwa mashamba na kila mmoja amepewa ekari tano (5) na hati ya umiliki ya miaka 66
    - Mafanikio ni pamoja na Uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika eneo lenye ukubwa wa ekari 220 kati ekari 1,772 umefikia asilimia 80.
    - Kumefanyika ujenzi wa bwawa lenye ujazo wa lita milioni 27 na na visima vinne (4) vimechimbwa kwa ajili ya umwagiliaji;
    - Ujenzi wa uzio kwa ajili ya kuzuia uvamizi wa shamba hilo umefika asilimia 89
    - Ujenzi wa kiwanda chenye uwezo wa kusindika zabibu tani 300 na kuhifadhi mchuzi wa zabibu lita 220,000 kwa mwaka umekamilika


2. **Shamba la Mlazo/Ndogowe**
    - Wizara imesafisha ekari 5,700 kati ya ekari 11,453 kwa ajili ya kuanza uzalishaji na usafishaji unaendelea
    - Ujenzi wa nyumba 53 umekamilika na ujenzi wa nyumba saba (7) umefikia wastani wa asilimia 92;
    - Vijana 342 wamepokelewa na kila kijana amepewa ekari 10 kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo;
    - Uchimbaji wa visima 11 na mabwawa nane (8) umefikia wastani wa asilimia 91;
    - Usimikaji na utandazaji wa mfumo wa umwagiliaji umefikia asilimia 65;
    - Ujenzi wa barabara za mashambani zenye urefu wa Kilomita 18.6 unaendelea; na
    - Ekari 2,500 amepewa Mwekezaji (Kampuni ya Longping Agriscience Tanzania Ltd) na atakuwa na jukumu la kutoa huduma ya teknolojia na ununuzi wa mazao yatakayozalishwa katika shamba hilo.

3 **Shamba la Mapogoro (Chunya- Mbeya)**

- Serikali imesaini makubaliano ya kupokea fedha kiasi cha Dola za Marekani Milioni 129 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi wa Mapogoro kwa kuanzia na hekta 20,000.
- Hadi Aprili 2025, Wizara imepata haki miliki ya mashamba hayo, imekamilisha upimaji wa afya ya udongo na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika shamba hilo.

### UPATIKANAJI WA MITAJI KWA VIJANA NA WANAWAKE (BBT - MITAJI)

Hadi kufikia April 2025, Wizara imefanikisha mambo yafauatayo kuongeza mitaji kwa vijana na wanawake:



- AGITF imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni 503.5 kwa vijana na wanawake;
- AGITF na TADB zimesaini hati ya makubaliano (MoU) ya kutumia mifumo ya dhamana ili kuzisaidia taasisi za fedha ziweze kuwakopesha vijana kwa kutumia dhamana zitakazosimamiwa na TADB.
- Vilevile, maombi ya mikopo 1,546 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 21.3 kwa ajili vijana na wanawake yamepokelewa na yapo kwenye hatua mbalimbali za kutolewa; na
- Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kupitia Mradi wa BBT project 1 unaofadhiliwa na AfDB

  inakamilisha majadiliano ya Dola za Marekani Milioni 35 kwa ajili ya dhamana na mikopo yenye riba nafuu kwa Vijana na Wanawake.
- Aidha tathmini itafanyika kwa ajili ya kuona uwezekano wa AGITF kutoa huduma hiyo kupitia Benki ya Ushirika Tanzania.

### MRADI WA HUDUMA ZA UGANI (BBT – UGANI)

Ajira 1,261 kwa wahitimu wa vyuo vikuu kutoa huduma za ugani

- jumla ya wahitimu wa vyuo vya kilimo 1,261 wamepata ajira ya kutoa huduma za ugani kwa wakulima katika mazao ya pamba (vijana 761) na Korosho (vijana 500).
- Pia, kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania tumeajiri vijana 108 kwa ajili ya kufundisha wakulima.

### MRADI WA VISIMA KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI (BBT – VISIMA)

hadi Aprili 2025, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

i. Imetangaza zabuni kwa ajili ya kununua uniti 250 za pampu, jenereta na mipira kwa ajili kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima waliopo kandokando ya Ziwa Victoria.

ii. Mradi huo unatarajia kunufaisha wakulima 10,000;

iii. Wizara Imebainisha maeneo ya kuchumba visima 39 vitakavyonufaisha wakulima zaidi ya 1,100

iv. Wizara inatekeleza ujenzi wa miradi midogo ya umwagiliaji (Community Irrigation) katika eneo lenye ukubwa wa ekari 4,000 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.68 inatekelezwa katika majimbo 62 na Halmashauri 58.

v. Wizara Imeanza uchimbaji wa visima 127 kwa kutumia wachimbaji wa ndani katika mikoa 16

### MRADI WA UONGEZAJI THAMANI YA MAZAO (BBT-VALUE ADDITION)

Vijana wenye mahitaji maalum wafikiwa na BBT

- Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya BBT kupitia mradi wa uongezaji thamani ya mazao ambapo kupitia Bodi ya Mkonge imeanzisha Kituo Atamizi cha Mkonge BBT katika Mkoa wa Tanga ili kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum/watu wenye walemavu kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia singa za Mkonge.
- Mradi huo unahusisha pande mbili (2) za Muungano za Tanzania Bara na Zanzibar ambapo vijana 344 wanaendelea na mafunzo ya kutengeza bidhaa zitokanazo na mkonge.
- mashine 66 zenye uwezo wa kubangua korosho kilo 20 kwa siku kwa kila moja zimesambazwa katika vikundi 12 vya wakulima.
- Pia, AGITF imetoa mikopo mitano (5) yenye thamani ya Shilingi Milioni 104.7 kwa vijana na wanawake kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya mahindi, mpunga na alizeti

### AJIRA MILIONI 3 KUZALISHWA KATI YA 2025-2030 NDANI YA BBT

"Wizara itaendelea kutekeleza kipaumbele cha kuchangia kuongeza ajira zenye staha kwa vijana na wanawake kufikia 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Ajira hizo zitatokana na utekelezaji wa Programu ya BBT kupitia miradi sita" Mhe. Hussein Mohammed Bashe, (Mb), Waziri wa Kilimo, Hotuba

ya Bajeti 2025/2026.

**MIRADI SITA YA KUZALISHA AJIRA ZA VIJANA MILIONI 3 IFIKAPO 2030**

i. (Wizara itaanza uwekezaji katika shamba la Mapogolo – Chunya (Mbeya) lenye ukubwa wa ekari 57,000 kwa kuanza na ekari 20,000 kwa kuandaa shamba, kujenga nyumba, miundombinu ya umwagiliaji na ghala.

ii. Kujenga ghala nane (8) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika mashamba ya Pamoja ya vijana ya Chinangali na Mlazo/Ndogowe

iii. Kujenga chumba cha baridi (cold room) chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika shamba la Chinangali

iv. Kujenga uzio wa umeme (km 27) kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe

Kuwezesha Uendelezaji wa programu ya BBT ngazi ya Halmashauri

- Kuendelea kutekeleza mradi wa BBT kwa kuanza na Halmashauri 20 zilizotenga maeneo yenye ukubwa wa kuanzia hekta 200 kwa kila Halmashauri; na
- Kuanzisha mashamba ya tumbaku yenye jumla ya ekari150 katika Halmashauri za Uyui na Chunya.

Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima Wadogo (BBT Visima)

- Kuchimba visima 500 vitakavyomwagilia kwenye mashamba ya wakulima wadogo eneo lenye ukubwa wa hekta 30,393.39 katika Halmashauri 178 nchini na kuwanufaisha wakulima 58,903
- Kuwekeza katika mashamba ya kahawa yenye jumla ya hekta 4,000 katika Mkoa wa kagera kwa kuchimba visima na kuwapatia zana za kilimo

Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana Wanawake (BBT Mitaji)

- AGITF kwa kushirikiana na benki ya Ushirika Tanzania
- itaanzisha dirisha maalum litakalotoa huduma za guarantee scheme, direct lending na equity fund kwa mikopo yenye riba nafuu na fedha za awali zitakazowekezwa ni kutoka AfDB kiasi cha Dola za Marekani Milioni 35.
- Pia, Wizara kupitia AGITF itaweka kiasi cha Shilingi Bilioni 17 katika dirisha la guarantee scheme ili kutoa mikopo yenye riba nafuu ya thamani ya Shilingi Bilioni 51 kwa wakulima kwa riba isiyozidi asilimia saba (7%)